



## Maswali na Majibu

1. Mungu alimtengeneza Adamu namna gani?  
*Kutoka kwa mchanga na akampulizia pumzi ya uhai kwa mapua*
2. Mungu alisema nini itafanyika Adamu na Hawa wakikataa kumtii?  
*Watakufa.*
3. Nini ilifanyika Adamu alipokufa?  
*Mungu alimtoa pumzi ya uhai na akarudi kwa mchanga.*
4. Mbona tunakufa?  
*Kwa sababu tumeienda dhambi.*
5. Biblia inafundisha kwamba mtu ana nafsi isiyokufa?  
*Hapana.*
6. Neno 'kuzimu' ina maana gani?  
*Kaburi.*
7. Jehanum ina maana gani?  
*Ni Bonde la Hinomu penye takataka za Yerusalemu zinatupwa na inakaa ikiwaka.*
8. Tunawezaje kuwa na tumaini la uzima baada ya kifo katika Yesu?  
*Dhambi zetu zinasamehewa kwa sababu Yesu alitoa uhai wake kama dhabihu. Kwa hivyo hatukai mautini milele.*
9. Wafu watafufuliwa lini?  
*Wakati Yesu atarudi kusimamisha Ufalme wa Mungu hapa duniani.*

## Mistari ya kukariri

Warumi 6:23      1 Wakorintho 15:22 – 23

## Mazungumzo

Tafuta mistari ifuatayo. Inatufundisha nini juu ya watu waliokufa?

Zaburi 6:5      Zaburi 146:4      Zaburi 39:13      Zaburi 115:17      Mhubiri 9:5

## Kuandika

Fafanua sababu tunakufa. Eleza tumaini letu katika Yesu ili tuokoke kutoka kwa kifo.

# Masomo ya watoto wakubwa wa CBM

## Somo la 4    Mtu ni wa kukufa

**SOMA**   **Yohana 3:16—17**

### SOMO

#### Dhambi na Adhabu

Hapo mwanzo Mungu aliumba mtu wa kwanza, Adamu. Mungu alitengeneza Adamu kutoka kwa mchanga wa chini. Mungu alimpulizia kwa mapua pumzi na akawa nafsi hai. Soma Mwanzo 2:7

Mungu alimtenezea Adamu bustani ya kuishi tena akamtengenezea mke. Mungu akampa Adamu amri zisiokuwa ngumu, "Kwa kweli unaweza kula matunda ya miti ingine yote ya bustani lakini usikule kutoka kwa mti wa ujuzi wa mema na maovu. Siku utakula hakika utakufa." (Mwanzo 2:16 – 17)

Adamu na Hawa walikuwa na uamuzi. Wangechagua kumtii Mungu au wasimtii. Walikuwa na uhuru wa kuchagua cha kufanya. Nyoka alimdanganya Hawa. Nyoka alisema hawatakuwa hata wakila tunda lililokatazwa. Hawa aliamini nyoka. Kwa hivyo Adamu na Hawa walichagua kumuasi Mungu na wakakula lile tunda. Walifanya dhambi kwa kutomtii Mungu.



Mungu alikuwa amesema watakuwa wakila lile tunda. Kwa hivyo Adamu na Hawa walihukumiwa kufa tena wakafukuzwa kutoka kwa bustani. Hata hivyo Adamu na Hawa waliishi miaka mingi baada ya kutenda dhambi, walikuwa ni wa kukufa – walichoka, waligonjwa na mwishowe walikuwa.

#### Kifo ni nini?

Kifo ni adhabu ya dhambi. Mungu alisema, "Wewe ni mchanga na kwa mchanga utarudi." (Mwanzo 3:19). Adamu alipokufa Mungu alimtoa pumzi ya uhai. Mwili wa Adamu ulioza na ukarudi kwa mchanga ulikotoka.

MCHANGA wa PUMZI = NAFSI HAI

MCHANGA bila pumzi = KIUMBE MFU

Adamu alikufa kwa sababu alitenda dhambi. Hata sisi tuko hivyo. Zote tumetenda dhambi kwa hivyo zote tunakufa. Tukifa, Mungu anachukuwa pumzi yetu na tunarudi kwa mchanga.  Soma Warumi 5:12

### Mashauri yasio ya kweli

Watu wengi hata leo wangali wanaamini uongo wenye nyoka aliambia Hawa, "Hakika hautakufa." Hawataki kuona au kufikiri kwamba kifo ni mwisho wao. Wanaamini kwamba wataendelea kuishi baada ya kifo.

Tafsiri ya Biblia zingine zinatumia neno NAFSI. Kwa mfano Mungu alipotengeneza Adamu inasema, "....mtu akawa *nafsi hai*. Hili neno 'nafsi' ina maana ya kiumbe, mtu au mnyama. Watu wengine wamechukuwa hili neno linamaana kwamba ni sehemu ya mtu inayoishi baada ya kufa. Wanaamini kuna nafsi isiyokufa. Hakuna kitu kama hicho kwamba kuna sehemu isiyokufa. Maneno eti nafsi inayoishi hayako kwa Biblia.

Biblia inafundisha kwamba kifo ni mshahara wa dhambi. Mungu anaondoa pumzi yake ya uhai na mwili unarudi kwa mchanga. Hakuna uhai unaobaki. Hakuna ufahamu wowote. Kifo ni mwisho wa uhai na hakuna sehemu inayoishi baada ya kufa.  Soma Mhubiri 9:5 – 6

### Mbinguni

Watu wengine wanaamini kwamba mtu akifa nafsi ya uhai inaenda Mbinguni kuishi na Mungu kwa sababu wana imani kwamba nafsi ya uhai lazima iende mahali baada ya kifo. Lakini kifo ni adhabu, na kuishi Mbinguni ni thawabu. Biblia haifundishi kwamba watu huenda Mbinguni wakifa. Kwanza Biblia hufunza kwamba hakuna aliyeenda mbinguni.  Soma Yohana 3:13. Daudi alikuwa karibu na moyo wa Mungu lakini Biblia inasema hakuenda mbinguni.  Soma Matendo 2:34.

Ikiwa tuna nafsi ya uhai, hakukuwa na maana ya Yesu kuja na afe ili atuokoe kutoka kwa dhambi. Watu wengi waliokaza kabla ya Yesu kuzaliwa wangekuwa tayari wanaishi mbinguni. Kama watu walikuwa na nafsi isiyokufa na wanaishi milele, Yesu hangekuja na afe kwa ajili yetu. Yesu alikufa kwa sababu wafu wanaacha kuwa hai. Wanawenza kuishi tena tu, wakati wa ufufuo kwa sababu Yesu alikufa kwa ajili yetu.

### Kuzimu

Kama watu wana nafsi isiyokufa inayoishi milele, ina maana kwamba waovu wana mahali pakuenda. Hawa watu wanaamini kwamba waovu wanaenda kuzimu ili wateswe kwa moto wa milele. Mungu wa upendo hawezu kutaka watu wateseke milele. Biblia inatufundisha kwamba waovu wanakufa na hawaishi tena. Hawateswi milele.

Biblia inazungumzia Kuzimu. Kwa hivyo kuzimu ni nini? Neno 'kuzimu' ni neno la kingereza cha zamani kumaanisha mahali 'palipojificha au palipofunikwa'. Inamaanisha kaburi. Kuzimu ni neno lingine la kaburi. Kuzimu ni kaburi. Tafsiri za Biblia za kisasa zinatumia zaidi neno kaburi badala ya kuzimu.

Na moto wa kuzimu je? Yesu anazungumzia hii kwa Marko 9:43 – 48. Alizungumzia kuzimu kwamba ni mahali ambapo moto hauzimiki. Alimaanisha nini? Neno 'kuzimu' kwa mistari hii ni 'Jehanum.' Ni neno la Kiebrania. Ni jina la Bonde. Jehanum ni Bonde la Hinomu (jina la mahali).

Bonde la Hinomu ni bonde liko inje ya Yerusalem. Wakati wa Yesu, Bonde la Hinomu lilikuwa ni mahali pa kutupa takataka zote za mji. Mizoga ya wanyama na takataka za mji zilitupwa huko. Moto uliwaka bila kugoma ukichoma – usiku na mchana. Palikuwa ni mahali pa uharibivu kabisa. Yesu alikuwa akimaanisha kwamba, waovu wakifa, wataharibiwa kabisa. Wataacha kuishi. HAKUMAANISHA kwamba watateswa milele.

### Mungu anatupa tumaini

Sisi zote tumehukumiwa kufa kwa sababu tu wenye dhambi. Hatuwezi kuwa hai kwa namna yoyote tukifa. Kwa hivyo tuna tumaini lolote? Hakuna tumaini lolote n'gambo ya kaburi?

Tumaini la kuishi baada ya kifo ni kupitia kwa Yesu Kristo. Kwa sababu Yesu aliishi bila dhambi na akapeana maisha yake kama dhabihu, tuna tumaini baada ya kifo.  Soma Yohana 3:16 – 17. Tusipokuwa na imani kwa Yesu, tutapotea – baada ya kufa hatutaishi tena milele. Lakini tukiamini kwa Yesu, Mungu atatupa maisha ya milele.

Tunasamehewa dhambi zetu kupitia kwa Yesu. Tunakufa kwa sababu tunadhambi. Dhambi zetu zikisamehewa kabisa na tuwe kama Yesu, hatutaishi mautini. Yesu atakapokuja hapa duniani atafufua wafu walioamini na kuwapa uzima wa milele.  Soma Yohana 6:40.

### Kufufuka kutoka kwa wafu

Tumaini la uzima baada ya kufa ni kufufuliwa kutoka kwa wafu wakati Yesu atakapo kuja kusimamisha Ufalme wa Mungu hapa duniani.  Soma Yohana 5:28 – 29. Danieli naye alizungumzia juu ya wafu kufufuliwa kwa uzima wa milele.  Soma Danieli 12:2

Tunakufa kwa sababu tu wenye dhambi. Lakini Mungu anatupenda hataki tupotee kabisa. Mungu alituma mwanawe wa pekee hapa duniani ili tuwe na tumaini la uzima wa milele. Tunasitahili kufa milele, lakini dhawabu ya Mungu katika Yesu ni uzima wa milele kwa Ufalme Wake duniani.  Soma Warumi 6:23